

ARCHITECTS AND QUANTITY SURVEYORS REGISTRATION BOARD
(Under Act No.4 of 2010)



TAARIFA KWA UMMA

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) ni taasisi ya serikali, chini ya Wizara ya Ujenzi, iliyoanzishwa chini ya sheria Na. 4 ya mwaka 2010.

Majukumu ya Bodi ni pamoja na kusajili Wabunifu Majengo (Architects), 'Interior Designers', 'Landscape Architects' Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors), 'Building Surveyors' na 'Construction Managers' na makampuni yao.

Aidha Bodi ina jukumu la kutembelea miradi ya ujenzi, ili kuhakikisha kuwa imebuniwa na kusimamiwa na Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi waliosajiliwa na Bodi.

Katika juhudi za Bodi za kuboresha mazingira jenzi (Built environment) inapenda kuwakumbusha wadau wote wa sekta ya ujenzi kuwa wanalazimika kisheria kuwahusisha Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi katika shughuli zao zote za ujenzi. Ni kosa la jinai chini ya kifungu 37(3) cha Sheria Na. 4 ya 2010 kujenga bila kuwa na wataalamu hao. Mwendelezaji atakaye kiuka hii sheria atapigwa faini isiyopungua Shs 5.0 Millions au 2% ya gharama ya ujenzi, kwa kuangalia iliyo kubwa au kifungu kisichopungua miaka mitatu(3), au vyote pamoja.

Aidha wahitimu wote wa fani za Ubunifu Majengo (Architecture), 'Interior Design', 'Landscape Architecture' 'Conservative Architecture' 'Naval Architecture', Ukadiriaji Majenzi (Quantity Surveying), 'Building Survey', 'Construction Management', Project Management', wanahimizwa kujisajili na Bodi katika ngazi ya utaalumu (professional) na utaalumu wa kati (semi - professionals). Fomu za kujisajili zinapatikana katika ofisi zetu zilizopo, Dar Es Salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza na Mbeya; pia katika tovuti ya Bodi, (www.aqrb.go.tz)

Usajili wa wataalamu wa kati(semi professionals) unafanyika katika kipindi kisichozidi siku tano, tangu siku ya kuwasilisha maombi kamili.

Ni kosa la jinai kwa mtu yeyote ambaye sio Mbunifu Majengo(Architects), Mkadiriaji Majenzi (Quantity Surveyor) au fani zinazoshabihiana nazo(allied disciplines) kufanya kazi za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi bila kusajiliwa na Bodi. Kwa mujibu wa kifungu Na. 34(1) cha sheria Na. 4 ya mwaka 2010. Atakaye bainika kutenda kosa hili atapigwa faini isiyopungua Shillingi 5.0 Million au kifungu kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Kwa ujenzi bora na salama, unaozingatia gharama halisi ya mradi, wananchi wanahimizwa kuwatumia Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na wataalamu wa fani zinazoshabihiana waliosajiliwa na Bodi.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Msajili,
Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi.
S.L.P. 72673
Simu: 2110292
Barua pepe: info@aqrb.go.tz, Tovuti: www.aqrb.go.tz
DAR ES SALAAM.